

## Elimu ya Ulinzi wa Watoto

### Habari kwa wazazi na walezi

Jina la shule  
Name of school

Mwaka/Miaka unayoshiriki  
Participating Year/s

Idadi ya masomo kwa wiki  
Number of lessons per week

Mtu wa mawasiliano wa shule  
School contact person

Nambari ya simu ya mawasiliano  
Contact telephone number

#### Wapendwa Wazazi na Walezi

Mwaka huu wanafunzi katika miaka iliyotajwa hapo juu watahusika katika somo la lazima la Maendeleo ya Kibinafsi, Afya na Elimu ya Kimwili (Personal Development, Health and Physical Education (PDHPE)).

Sehemu ya mpango wa PDHPE wa shule yetu ni pamoja na elimu ya lazima ya ulinzi wa watoto. Baadhi ya mada yanayofundishwa katika elimu ya ulinzi wa watoto hushughulikia maswala nyeti. Shule itafundisha mada hiyo kwa njia ya kufaa kwa umri.

Yaliyomo maalum ambayo yatafundishwa katika elimu ya ulinzi wa watoto ymeonyeshwa kwenye ukurasa unaofuata.

Kwa habari zaidi juu ya elimu ya ulinzi wa watoto nenda kwa sehemu ya [Child protection and respectful relationships education](#) (Elimu ya ulinzi wa watoto na ya uhusiano wa heshima) kwenye tovuti ya Idara ya Elimu ya PDHPE.

Idadi ya masomo kwa wiki katika kipindi hiki ambayo elimu ya ulinzi wa watoto itafundishwa huonyeshwa hapo juu.

Ikiwa ungependa habari zaidi, tafadhali wasiliana na mtu wa mawasiliano wa shule ambaye jina pamoja na nambari ya simu inaonyeshwa hapo juu.

### Huduma ya Ukalimani wa Simu

Ikiwa unahitaji mkalimani kukusaidia kuwasiliana na shule, tafadhali piga simu Huduma ya Ukalimani wa Simu kwenye 13 14 50 na uombe mkalimani kwa lugha yako. Operata atapiga simu shuleni na kupata mkalimani kwenye laini kusaidia mazungumzo. Hutatozwa kwa huduma hii.

Mwaminifu wako

Mwalimu Mkuu (Principal)

Yaliyomo katika elimu ya ulinzi ya watoto ni pamoja na:

The content which will be covered in child protection education includes:

(Staff to tick the relevant boxes below for Early Stage 1 content.)

Hisia na athari za mwili  
Feelings and body reactions

Mahusiano na wengine  
Relationships with others

Jinsi watu wanavyotunzana  
How people care for each other

Sehemu za mwili (za siri na za kawaida)  
Body parts (private and non-private)

Mabadiliko katika mwili na uwezo tangu kuzaliwa  
Changes in body and abilities since birth

Haki na majukumu  
Rights and responsibilities

Miundo ya familia  
Family structures

Kutambua na kujibu hali salama na zisizo salama  
Recognising and responding to safe and unsafe situations

Mahusiano mazuri na mitandao ya msaada  
Positive relationships and support networks

Mikakati ya kukaa salama na kuomba msaada  
Strategies to stay safe and ask for help

Ugusaji ambao unafaa na usiofaa  
Appropriate and inappropriate touching

Njia za kuonyesha heshima kwa wengine  
Ways to show respect to others

Kuamua maamuzi salama  
Making safe decisions